



Bibilia ya watoto
Inaleta

Mungu alipoumba
kila kitu



Kimeandikwa na: E. Duncan Hughes
Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus
Imerekebishwa na: Bob Davies; Tammy S.
Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2008 Bible for Children, Inc.


License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Ni nani aliyetuumba? Bibilia, Neno la Mungu, linatueleza jinzi viumbe vyote alivyoanza. Hapo mwanzo Mungu aliumba mwanadamu wa kwanza akamuita Adamu. Mungu alimuumba Adamu kutoka kwa mavumbi ya ardhi. Mungu alipopuliza uhai ndani ya Adamu, alikuwa hai. Akijipata katika bustani maridadi ya Edeni.




Kabla Mungu kumuumba Adamu, aliumba ulimwengu maridadi uliojazwe na vitu vya kustaajabisha. Hatua baada ya nyingine Mungu alifanya vilima na anga, maua ya manukato mazuri, na miti mirefu, ndege wa angani na nyuki, samaki wa majini na konokono.



Ama kweli, Mungu ndiye aliyeumba vyote vionekavyo.



Hapo mwanzo, kabla
Mungu kuumba
chochote, hakukuwa na
chochote ila Mungu.
Hapakuwa na watu
ama, mahala popote
au vitu vyovyote. La.
Hapana mwanga wala
giza. Hapakuwa na
milima wala mabonde.
Jana na kesho
hazikuwepo. Palikuwa
tu Mungu asiyekuwa na
mwanzo. Mungu
akajukuwa hatua.




Hapo mwanzo
Mungu aliumba
mbingu na nchi.




Na nchi ilikuwa
ukiwa, tena utupu.
Na giza ilikuwa
juu ya vilindi
vya maji.
Kishi Mungu
akasema,
"Iwe
nuru."



Pakawa nuru. Mungu akaita nuru Mchana na giza akaita Usiku. Jioni na asubuhi hiyo ikawa siku ya kwanza.



Kwenye siku ya pili, Mungu akayaweka maji ya bahari, ziwa na mito kwa mpangilio chini ya mbingu. Siku ya tatu, Mungu akasema, maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hivyo.




Mungu akaiamuru nchi kutoa majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo. Ikawa jioni, ikiwa asubuhi, siku ya tatu.



Mungu akafanya jua, mwezi na nyota
nyingi zisizo hesabika. Ikawa jino na
asubuhi siku ya nne.




Viumbe vya bahari,
samaki na ndege ndivyo
vilivyo fuatilia kwa
orodha ya Mungu. Siku
ya tano Mungu akaumba
nyangumi wakubwa na
akila kiumbe chenye uhai
kiendacho, ambavyo maji
yalijawa navyo kwa wingi
kwa jinsi zao, na kila
ndege arukaye, kwa jinsi
yake; ikawa jioni, ikawa
asubuhi siku ya tano.




Baada ya hayo, Mungu akanena tena, akasema,
"Nchi na iza e kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa
kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwito
kwa jinsi zake; ikawa hivyo."

Ikawa jioni, ikawa asubuhi siku ya sita.




Mungu alifanya kitu kingine tofauti kwa siku ya sita - kitu cha maana sana. Vitu vyote vilikuwa tayari kwa mwanadamu. Viakula vilikuwa mashambani na wanyama wa kumtumikia, Mungu akasema,

"Natufanye mtu kwa mfano wetu. Na awe mtawala wa vitu vyote nchini." **BASI MUNGU AKAUMBA MTU KWA MFANO WAKE; KWA MFANO WA MUNGU ALIMUUMBA....**




Mungu akanena na Adamu. "Kula chochote utakacho kutoka kwenye bustani. Lakini usile kutoka kwenye mti wa ujuzi wa kujua mema na mabaya. Mkila kutoka kwa mti huo hakika mtakufa."



Bwana Mungu akasema, "Si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanya msaidizi wa kufanana naye." Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndili jina lake.




Adamu akawapa majina wote. Alikuwa mwerevu sana kwa kutenda haya. Lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye.



Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, Mungu akafanya mwanamke kutoka kwa

ubavu huo. Mwanamke huyu aliyeumbwa na Mungu alikuwa msaidizi wa kufanana na Adamu.



Kwa siku sita Mungu aliumba vitu vyote.
Mungu akaibariki siku ya saba na kuiweka
siku ya mapumziko. Katika bustani la Edeni,
Adamu na mkewe Hawa walikuwa na furaha
kamilifu kumutii Mungu. Mungu alikuwa
Bwana wao, msaidizi na rafiki wao.



Mungu alipoumba kila kitu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mwanzo 1-2


"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130





1



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

